

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

**MAOMBI YA KUPIGIWA KURA KWA MIRADI YA TEHAMA
ILYOCHAGULIWA KUSHINDANA KWENYE TUZO ZA WSIS 2026**

Kufuatia Taarifa kwa Umma iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) tarehe 5 Februari, 2026 juu ya wito wa kushiriki katika tuzo za WSIS, picha bora na uwasilishaji wa miradi ya TEHAMA kwa mwaka 2026, TCRA kama mratibu inawashukuru wadau wote waliowasilisha miradi yao, na tunayo furaha kuwajulisha umma kwa ujumla na wadau wa WSIS kuwa miradi nane (8) kutoka Tanzania imechaguliwa kwa hatua ya kupigiwa kura.

TCRA inahimiza Umma kwa ujumla, zikiwemo taasisi za Serikali, sekta binafsi, taasisi za kimataifa na kikanda, asasi za kiraia na wanataaluma kupigia kura miradi hii kabla au ifikapo 3 Mei, 2026 ili kuipa nafasi miradi ya Tanzania kushinda tuzo hizi muhimu.

Orodha ya miradi iliyochanguliwa kutoka Tanzania kwa Tuzo za WSIS 2026

S/N	Na. Lengo	Lengo	Jina la Mradi	Taasisi
1.	Lengo Na. 1 la WSIS (AL C1)	Nafasi ya Serikali na wadau mbalimbali katika kukuza TEHAMA kwa maendeleo. The role of governments and all stakeholders in the promotion of ICTs for development.	Mradi wa Jamii Stack (National Digital Public Infrastructure).	Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
2.	Lengo Na. 1 la WSIS (AL C1)	Nafasi ya Serikali na wadau mbalimbali katika kukuza TEHAMA kwa maendeleo. The role of governments and all stakeholders in the promotion of ICTs for development.	Mradi wa Mapinduzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma kupitia Mfumo wa Mipango, Bajeti na Utoaji Taarifa unaoendeshwa na Akili Undwe (AI). PlanRep v2.0 – Transforming Public Finance through AI-Driven Decentralized Planning, Budgeting and Reporting System.	Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM–TAMISEMI)

S/N	Na. Lengo	Lengo	Jina la Mradi	Taasisi
3.	Lengo Na. 2 la WSIS (AL C2)	Miundombinu ya TEHAMA. Information and communication infrastructure.	Mradi wa Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano 758. Construction of 758 Telecom Towers under Digital Tanzania Project.	Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)
4.	Lengo Na. 3 la WSIS (AL C1)	Upatikanaji wa habari na ujuzi Access to information and knowledge.	Mradi wa Ushirikishwaji wa Kidijitali Tanzania. Aiphabet and Child Online Africa Launch AI Literacy Initiative.	Aiphabet (USA – Civil Society) in partnership with Child Online Africa
5.	Lengo Na. 5 la WSIS (AL C5)	Kuimarisha imani na usalama katika kutumia TEHAMA. Building confidence and security in use of ICT.	Shindano la Cyber Champions (Cyber Champions Competition)	Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)
6.	Lengo Na. 7 la WSIS (AL C7)	Serikali Mtandao (E-Government)	Mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi wa Kielektroniki wa Tanzania (NeST) – Mageuzi na Mustakabali wa NeST. National e-Procurement System of Tanzania (NeST) – The Evolution and Future of NeST	Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA)
7.	Lengo Na. 7 la WSIS (AL C7)	E-Environment	Mradi wa Taka za Kielektroniki. Tanzania (E-TAP) E-Waste Tanzania Project (E-TAP).	Asasi ya Kirai ya UMKITA
8.	Lengo Na. 8 la WSIS (AL C8)	Utofauti wa kitamaduni na utambulisho, utofauti wa lugha na maudhui ya ndani Cultural diversity and identity, linguistic diversity and local content	TEHAMA kwa Viziwi. ICT for the Deaf.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania – Kituo cha Ubunifu

Taratibu za Kupiga Kura

- Ili kupiga Kura tumia kiunganishi hiki <https://www.itu.int/net4/wsis/stocktaking/Prizes/Prizes> kujisajili kwenye Jukwaa la WSIS chini ya Tuzo za WSIS 2026.
- Jisajili kwa kutumia baruapepe yako ambayo pia utaitumia kuingia kwenye mfumo.
- Baada ya kuingia, nenda kwenye sehemu ya kupiga kura imeandikwa "Vote", utaletewa orodha ya miradi kulingana na lengo (category) kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la miradi nane (8) iliyochaguliwa kutoka Tanzania.
- Chagua jina la lengo (category) kisha chagua miradi husika na upige kura kwa kubofya "Vote for this Project" upande wa kulia wa mradi husika.

Tafadhali Kumbuka masharti yafuatayo

- Siku ya mwisho ya kupiga kura ni **3 Mei, 2026**, baada ya hapo washindi (90) wa Tuzo za WSIS 2026 watatangazwa na kutambuliwa katika Hatua ya Uteuzi.
- Kila mwanachama anaweza kupiga kura mradi mmoja tu katika kila lengo.
- Taasisi haziruhusiwi kuupigia kura mradi wao wenyewe.

Ukomo wa kupiga kura ni **tarehe 3 Mei, 2026**.

Imetolewa tarehe **28 Aprili, 2026**.



Mha. Peter P. Mwasalyanda
MKURUGENZI MKUU